JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MKOA NA SERIKALI ZA MITAA.

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA.

SHULE YA SEKONDARI BARUTI,

S.L.P 540,

MUSOMA.

……………………….

KUMB.Na/HMM/SSB/K.I/2020/

MWANAFUNZI……………………………………………………………….

S.L.P …………

MUSOMA.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BARUTI HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA MWAKA 2021.

1.1 Nafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Baruti mwaka 2021. Shule ipo katika halmashauri ya manispaa ya Musoma, kata ya Nyakato kwenye mbuga iliyo jirani na ofisi za **SIDO**. Shule iko umbali wa takribani km 2 kutoka mjini kandokando ya barabara inayoelekea Mwanza. Muhula wa kwanza wa masomo unatarajiwa kuanza tarehe 11/01/2021 saa 1:00 asubuhi. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 ukiwa na vifaa vyote vya darasani ulivyoandikiwa katika fomu hii ili kuwa tayari kuanza mafunzo ya ENGLISH ORIENTATION COURSE. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 25/01/2021 zaidi ya hapo hautapokelewa isipokuwa kwa kibali cha Afisa Elimu

1.2 SARE YA SHULE.

**WASICHANA:**

a) Mashati/Blauzi mbili (2) nyeupe zenye alama ya **I (moja ya kirumi)** ya rangi ya damu yam zee kwenye bega la kushoto.

b) Sketi mbili (2) rangi ya damu yam zee kitambaa kizito, ziwe ndefu inchi 6 kutoka kwenye kisigino cha viatu (chini) kwenye pindo la chini la sketi. Ziwe na mistari (michirizi) mweupe wenye upana wa sentimita moja (1) na upana kati ya mstari mmoja na mwingine iwe sentimeta mbili (2). Mistari (michirizi) iwe mbele ya sketi inayotelemka chini kuanzia pindo la juu hadi chini.

c) Soksi nyeupe jozi mbili (2).

d) Viatu vyeusi jozi mbili (2) vya ngozi vya kamba na view na visigino vifupi.

e) Tai ndefu ya rangi ya damu yam zee.

f) Raba za michezo.

g) Bukta ya michezo ya rangi nyekundu.

h) Sweta rangi ya damu yam zee lenye alama ya **I (moja ya kirumi)** rangi nyeupe kwenye bega la kushoto.

**NB**: Wanafunzi wa kiislamu wa kike hawataruhusiwa kuvaa suruali shuleni.

**WAVULANA**:

a) Suruali mbili (2) rangi ya damu yam zee zishonwe kwa hadhi na siyo aina ya danglizi, jeans au isiwe ya kubana(modo). Upana wa chini uweze kupita kwenye goti lako bila kubana.

b) Mashati mawili (2) meupe yenye alama **I (moja ya kirumi)** ya rangi ya damu yam zee kwenye bega la kushoto.

c) Viatu jozi mbili (2) vyeusi vya ngozi vya kamba na visiwe vimechongoka kwa mbele.

d) Tai ndefu ya rangi ya damu yam zee.

e) Mkanda mweusi wa ngozi.

f) Soksi nyeupe jozi mbili (2).

g) Raba za michezo.

h) Bukta ya michezo ya rangi ya bluu.

i) Sweta rangi ya damu yam zee lenye alama ya **I (moja ya kirumi)** rangi nyeupe kwenye bega la kushoto.

1.3 VIFAA VYA DARASANI:

a) Mathematical set (bofa).

b) Madaftari ya kutosha kwa masomo tisa (9), rula, kalamu, penseli na mfumo wa kubebea madaftari.

c) Kamusi ya lugha ya kingereza kwa matumizi ya mwanafunzi mwenyewe.

d) Vitabu vya masomo mbalimbali vya kiada na ziada kwa ajili ya kujiongezea maarifa mwanafunzi.

2.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

2.1 Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sharia ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo ndiyo utakuwa mwongozo wako kukuwezesha kukaa hapa shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wote na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani nan je ya shule ni muhimu.

c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa shuleni.

d) Unatakiwa kuangalia na kutunza dawati na kiti utakachokabidhiwa hapa shuleni wakati wowote wa uanafunzi wako hapa shuleni na utakabidhi kwa mwalimu wa darasa siku ukihitimu au kuhama shule.

e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako shuleni hapa.

f) Kufanya mazoezi ya darasani na mitihani yote ya ndani nan je.

g) Kutunza usafi wa mazingira ya shule yako na mwili.

h) Kuvaa kikamilifu sare ya shule wakati wote unaopaswa kufanya hivyo.

i) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote wa uanafunzi wako.

2.2 **MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUKUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE.**

1. Wizi.
2. Utoro uliokithiri.
3. Uasherati na ushoga.
4. Ubakaji.
5. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine, mirungi n.k
6. Kupigana au kupiga.
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
8. Kudharau bendera ya taifa.
9. Kuoa au kuolewa.
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
11. Kutoa mimba.

12. Kugoma, kuchochea au kuongoza kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.
14. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi shuleni.

**Nakutakia maandalizi mema unapojiandaa kujiunga na shule ya sekondari Baruti**

Karibu sana katika shule hii.

Kauli mbiu: **EDUCATION IS A KEY TO SUCCESS**.(*Elimu ni ufunguo wa mafanikio).*

NB: Jaza viambatisho "A" kikamilifu kabla ya kuvirejesha hapa shuleni siku ya kuripoti.